

**SALAAM YA JUMAPILI YA UDUGU SEPTEMBA 20, 2020 KUTOKA
JIMBO LA KASKAZINI B (MISSENYE) – KKKKT / DKMG, TANZANIA**

Wependwa dada na kaka zetu katika Jimbo rafiki la Lüdenscheid-Plettenberg, Ujerumani.

Kwa niaba ya ndugu zenu wa Jimbo la Kaskazini B (Missenye) Tanzania, nawa salimuni nyote katika Jina la Bwana na Mkombozi wetu Yesu Kristo.

Leo tunasherehekeea Jumapili ya Udugu ikiwa ni miaka 36 tangu udugu wetu ulipoanzishwa. Kwa kipindi hicho chote udugu wetu umekua na kuenea sehemu mbalimbali za Majimbo yetu huku matunda yake yakionekana dhahiri.

Mwaka huu majimbo yetu pamoja na mambo mengine yamekuwa na mabadiliko ya uongozi. Jimbo la Kaskazini B limekuwa na kiongozi mpya tangu Februari, 2020. Habari tulizo nazo ni kwamba katika Jimbo lenu pia atachaguliwa Mchungaji wa Jimbo mpya mwezi huu wa Septemba, 2020. Mungu atusaidie viongozi wapya kwa kushirikiana na wengine kuendeleza udugu wetu kwa mafanikio. Tunakumbuka kwa shukrani kazi kubwa na nzuri ya Mchungaji wa Jimbo aliystaa fu, Claus Majoreess katika kuendeleza na kuimarisha udugu wetu. Mungu ambariki na kumtunza katika uzee wake.

Hapa Jimboni pamoja na kwamba Jumapili ya udugu itaazimishwa katika Mitaa yote Jimboni; Kijimbo itaadhimishwa katika Mtaa mdogo wa Kyabunaga, Usharika Bugango. Tunazo sababu zifuatazo za kufanya hivyo:-

- i. Huu ni Mtaa mpya ulioanzishwa mwaka 2016.
- ii. Mtaa huu una wajibu wa ujenzi wa Kanisa jipya la kudumu. Kwa njia ya Ibada hii tunapenda kuwapatia mwamko mpya kutoka ngazi ya Jimbo.
- iii. Katika maeneo haya wanaishi watu wa madhehebu na dini mbalimbali. Tunapenda Ibada hii iwe ishara ya kuishiana na kukua kwa pamoja.

Salaam yangu maalumu kwenu ni wazo kuu la kalenda yetu wiki hii lisemalo:

Mungu hututunza kwa uwezo wake mkuu likihusianishwa na Neno la Mungu kutoka Mk. 7:31 – 37. Wazo hili kuu linasema mambo mawili kuhusu Mungu:-


Mungu hututunza: Suala la Mungu kututunza liko wazi. Maisha yetu mara kwa mara yanakabiliwa na hatari mbalimbali kama vile ajali, magonjwa makali, misukosuko n.k ambapo kama si Mungu kututunza, kutufariji na kutubeba kwa muda mwingu kwa upande wetu tusingelisalimika.

Mungu ana uwezo: Kila kitu na kila jambo liko chini ya uwezo wake na hivyo, anapotenda lolote ana mamlaka yote. Somo hili linatudhihilishia utunzaji na uweza wake Mungu katika habari ya Bwana Yesu kumponya mpagani kiziwi - bubu.

Wakati huu wa ugonjwa wa Korona ulioenea dunia nzima tumekutana na changamoto nyingi. Katika changamoto hizi mmesimama nasi kutuwezesha kuendelea kutoa elimu kwa washarika na viongozi ya namna ya kujikinga na ugonjwa huu hatari. Tuendelee kushirikiana kuwatia moyo, kuwaombea na kuwafariji waathirika na wote waliopoteza ndugu zao kutoptana na ugonjwa huu, bila kusahahu kuchukua tahadhari tunazoelekezwa na wataalamu wetu wa afya. Katikati ya changamoto mbalimbali tunazokutana nazo sauti ya Mungu inetuelekeza ikisema: "... **waambie wana wa Israeli waendeleee mbele**" Kutoka 14:15b. Kwa maneno haya ni kama Mungu anasema, hakuna sababu ya kuogopa kwa kuwa yeye yupo pamoja na watu wake safarini kuwaongoza na kuwatunza. Nasi tumeshuhudia uongozi wake na utunzaji wake katika maisha yetu ya kila siku na hata katika wakati huu wa ugonjwa huu wa korona.

"Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu". Wafilipi 4:7.

Bwana awabariki na abariki kazi yake inayoendelea katika majimbo yetu.


Mchg. Arnold N. Mdogo

MCHUNGAJI WA JIMBO – KASKAZINI B.

